



**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**



**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUAHIRISHWA KWA ZOEZI LA AJIRA ZA WATUMISHI WA  
MUDA KWA AJILI YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA  
KUDUMU LA WAPIGA KURA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwataarifu Wananchi wote kuwa tarehe 30 Mei, 2019 iliwatangazia nafasi za kazi za muda kupitia tovuti yake ya [www.nec.go.tz](http://www.nec.go.tz) na kuwaalika watanzania wenye sifa zilizo ainishwa kwenye tangazo hilo kuomba nafasi hizo za kazi.

Hivyo, Tume inapenda kuwataarifu wananchi wote ya kwamba mchakato wa ajira za muda kwa ajili ya zoezi hilo umeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena.

Aidha, Tume inapenda kutoa shukrani zake kwa wale wote walioleta maombi yao ya kazi na inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

**Dkt. Athumani Kihamia**

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**